

List of characters by scene:

SCENE ONE: CHIVASI AND LINDA IN A CAFETERIA IN TOWN

- Linda (f, 20)
- Chivasi (m, 22)

SCENE TWO: FARAHANI AND SULE COMING FROM PRAYERS

- Farahani (m, 19)
- Sule (m, 19)

SCENE THREE: EVENING AT LINDA'S HOUSE

- Linda (f, 20)
- Mr. Maraga (m, 60)
- Mrs. Maraga (f, 55)

INTRO:

Hujambo msikilizaji na Karibu katika msururu wa vipindi hivi vya Learning By Ear “Noa Bongo Jenga Maisha Yako” Huu ni mfululizo wa vipindi vipya kabisa vya mchezo wa redio kuhusu **uhamiaji.....** katika kile kiinachoaminika kuwa “**Ardhi ya Ahadi – Hadithi kuhusu Waafrika wanaohamia Bara Ulaya**” Hii ni tamthilia inayoelezea maisha ya Wa-Afrika wanaohamia mataifa ya kigeni kutafuta maisha bora. Na siku haiwezi pita bila ya habari kuhusu wahamiaji wasio halali kutoka Afrika na sehemu nyinginezo Ulimwenguni, wakiwasili katika fukwe za bahari ya mataifa ya bara Ulaya kutafuta maisha bora. Wahamiaji hawa huhatarisha maisha yao kufika bara Ulaya. Na sio wahamiaji haramu pekee bali hata wale halali wanaoingia Ulaya. Nini hasa kichowachochea Wa-Afrika kuhama nchi zao na kuelekea Ulaya? Na nini hatima wanapowasili huko Ulaya? Ili kupata majibu ya maswali haya, tega sikio katika sehemu hii ya Kwanza **NDOTO YA MAISHA BORA YA KESHO**. Katika sehemu hii ya kwanza, tunakutana na vijana kutoka sehemu mbali mbali barani Afrika. Chivasi na Linda ni marafiki wa tangu utotoni kutoka

matafia yaliyoko kusini mwa Jangwa la Sahara. Sasa wamekuwa watu wazima, na baada ya kufuzu chuo kikuu, wanaamua kuishi pamoja katika maisha ya ndoa. Japo Chivasi yuko tayari kuishi maisha haya ya ndoa, wazazi wa Linda bado wanasita na wanapinga tofauti kabisa. Je ni vipi watakabiliana na changamoto hizi? Endelea kuwa nasi usikie hadithi yao wanapokutana katika mkahawa mmoja mjini.

SCENE ONE: CHIVASI AND LINDA IN A CAFETERIA IN TOWN

1. SFX: BUSY CAFE ATMO

2. CHIVASI: (eats and smacks his lips) Linda, unawaza nini?
Fikira zako ziko mbali sana.

3. LINDA: Chivasi...nina...ehh Sijui nianze vipi?

4. CHIVASI: (with his mouth full) Mmmh...ni habari njema au?
Yaonekana ni jambo zito sana. Usiwe na hofu mpenzi wangu. Ndio mwanzo tumemaliza masomo yetu na sasa nikusubiri matokeo. Nadhani hatutasumbuka kutafuta kazi.

5. LINDA: (cuts him short) Nataka kusafiri ng'ambo!.

6. CHIVASI: (swallows and coughs, shocked) Nini?! Linda, unasema nini?

7. SFX: FORK FALLS ONTO PLATE

- 8. LINDA:** Chivasi, Usiwe na wasi wasi . Nakwenda Ulaya kuendelea na masomo yangu.
- 9. CHIVASI:** **(utterly shocked)** Hapana!,haiwezekani Linda. Huwezi kunifanya hivyo!. Taadhali usiende ng'ambo nakuomba ubakie hapa hapa nyumbani!.
- 10. LINDA:** Wazazi wangu tayari wameamua Chivasi na siwezi kwenda kinyume na matakwa yao. Wanasema kuwa ukisomea Ulaya utakuwa na nafasi nzuri katika soko la ajira.
- 11. CHIVASI:** **(heartbroken)** Na mimi je? Nakupenda sana Linda! Kwa hiyo unataka nikusahau kabisa.
- 12. LINDA:** Chivasi! Kwanini unasema hivyo? Siendi kabisa!. Ni muda wa miaka mitatu tu kisha nitarejea!. Unafahamu jinsi gani nitaka kuwa nawe.
- 13. CHIVASI:** **(even more shocked)** Miaka mitatu ! Linda, miaka mitatu ni muda mrefu.
- 14. LINDA:** Chivasi, usifikirie hivyo. Hii ni faida kwetu sote!. Kwa maisha yetu ya baadaye. Mbali na hayo, tunaweza pia kuwasiliana kupitia mtandao wa facebook. Hii ni rahisi, ni kama tuko pamoja tu, na muda huo utasonga

haraka sana. Ukitafakari nitakuwa nimerudi nyumbani kuwa na wewe tena.

15. CHIVASI: Nitakuamini vipi Linda, kama

16. LINDA: Kama nini?

17. CHIVASI: Kama unaahidi tuoane utakaporudi.

18. LINDA: Chivasi sidhani ni vyema kutoa ahadi hiyo .

19. CHIVASI: Kama kweli wanipenda kama unavyodai, basi nipe ahadi. Nami nitakusubiri.

20. LINDA: **(confused)** Chivasi...Siwezi! Samahani lakini sioni naweza kukupa ahadi hiyo. Watu wengi wameweka matumaini makubwa kwangu... **(almost in tears)**

21. SFX: DINING CHAIR BEING PULLED BACK

22. CHIVASI: **(shouts)** Linda! Linda! Unaenda wapi? Linda!

23. SFX: HURRIED FOOTSTEPS LEAVING

24. NARRATOR: Huu ndio mtanziko unaopata watu kila siku barani. Kujikuta katika njia panda huku wakijiuliza maswali, Je niache nchi yangu, mke au mume wangu, na maisha niliyoyazowea, kwenda kuishi maisha nisiyoyafahamu katika nchi ya kigeni?" Ukweli ni kwamba, ingawa baadhi

yao huamua kubakia nchini mwao, wengi ni wale wanaokata shauri ya kuhamia kwi nchineko. Je! Linda atafanya nini baada ya kuondoka kwa hasira katika makahwa alikokuwa na miadi ya chakula cha mchana na Chivasi? Ili kupanda uhondo zaidi endelea kuwa nasi. Lakini sasa tunasafiri hadi Afrika Kaskazini ambako tunakutana na Farahani ambaye ni yatima. Rafiki yake Sule pia anatoka familia ya Wavuvi. Wote hawa hawana ajira, na ndoto yao ni moja tu, kuhamia Ulaya.

SCENE TWO: FARAHANI AND SULE COMING FROM PRAYERS

25. SFX: Market atmosphere, muezzin calling from a mosque in the background

26. SULE: (cheerful) Farahani, unawaza nini?

27. FARAHANI: (absent-minded) Huh? ... Usijali. Si jambo muhimu.

28. SULE: (concerned) Una uhakika. Siku hizi umenyamaza sana. Una tatizo gani?

29. FARAHANI: Ah, Sule, mara nyingine huwa na waza sana lini tutapata amani nchini mwetu? Mizozo, chuki, kulipiziana kisasi... Nimewapoteza wazazi wangu kwa sababu hii Sule. Nimechukia sana maisha haya, Hebu twende kule chini ufuoni.....

30. SULE: (cuts him short) Baharini? Tena? Farahani, naelewa

ni jinsi gani unavyotamani maisha ya Ulaya. Mimi pia!,
Lakini hapa ndipo tulipozaliwa.

31. FARAHANI: (**adamant**) Hapana! Hapa hakuna maisha mazuri,
Ulaya ndio watu wanaishi maisha ya sawa sawa!

32. SULE: Nini? Yaaani hakuna maisha hapa?. Kwani tumekufa
Farahani? Mbona waishi vizuri tu!

33. FARAHANI: Sule, Sio eti tumekufa, lakini haya si maisha. (**pause**)
Nikuhangaika tu!.

34. SULE: Kuhangaika?.

35. FARAHANI: (**emphatic**)Yes Ndio,maisha ya kung'ang'ana kila siku.
Lakini nasikia, maisha ni mazuri, mara mia moja
barani Ulaya. Huko mtu ana matumaini ya siku za
usoni, sio kama hapa kuchomwa kila siku. Mtu akifaulu
kwenda Ulaya, basi maisha yanabadilika mara moja.
Hebu twende ufuoni tukatazame mwangaza wa
Ulaya!.

36. SULE: Ah, wacha wewe na hoja zako za mwangaza wa
Ulaya!. Haya sawa twende.

37. FARAHANI: Sule, Siku moja nitafanikiwa kuvuka upande ule
mwingine wa Dunia, na naaamini yatanibadilikia.

38. NARRATOR: Hii ndiyo ndoto ya Farahani, Sule na vijana wengine wengi kutoka Afrika kuhamia Ulaya. Je! ni makosa kwa vijana hawa kuwa na ndoto ya aina hii? Tafakari hayo wakati hadithi yetu inapoendelea. Baadaye jioni siku hiyo nyumbani kwa familia ya Linda tunakutana na Bw. na Bi. Maraga wakiwa na furaha isiyo kifani.

SCENE THREE: EVENING AT LINDA'S HOUSE

39. SFX: HOT DRINK BEING POURED INTO A CUP

40. MR. MARAGA: Asante sana Linda! Je umemfahamisha Chivasi kwamba unaenda Ulaya kwa masomo zaidi?

41. MRS. MARAGA: Ndiyo, mimi pia nimekuwa nikilifikiria sana suala hilo. Leo nyinyi wawili mlikuwa pamoja kwa chakula cha mchana , sivyo?

42. LINDA: **(surprised)** Mh! Umejuaje? Kwani unatuchunguza?

43. MRS. MARAGA: Mmm... Ndiyo!.Kwenye mtandao wa Facebook. Mambo yote yako wazi! Taarifa ya hivi punde kabisa kwenye ukurasa wake, Chivasi anasema: **(mimics Chivasi's voice)** "Msinisumbue, leo nina miadi na mpenzi wangu wa pekee kwa chakula cha mchana."

44. MR. MARAGA: Ah, vijana wa sasa!. Hamwezi hata kidogo kuweka siri juu ya mambo yenu!.

45. LINDA: (bitter) Lakini si vizuri.

46. MR. MARAGA: Linda! Si vizuri nini?

47. LINDA: Kwani kunipeleka Ulaya, nikusema nisahau yote ya nyumbani?

48. MRS. MARAGA: Ndiyo! Hakuna! Hamna lolote hapa nchini mwetu. Ni umaskini tu, na hali ya kukata tamaa maishani!.

49. MR. MARAGA: (angrily) Mama Linda, hebu mpe nafasi Binti yetu ajieleze!

50. (short silence)

51. MR. MARAGA: Linda, Unasema nini...?

52. LINDA: Baba ...mama... najua mwanitakia mema, nami nawashukuru kwa hilo! Lakini tayari safari yangu ya kwenda ng'ambo imetatiza mipango yetu na Chivasi.

53. MR. MARAGA: (curiously) Imetatiza vipi, Linda? Kwani anatisha kukuacha baada ya ya kumwambia habari hizi njema?

54. LINDA: Ndilo tatizo kubwa hilo, Baba! Hii ni habari njema kwenu lakini sio kwa kila mtu. Chivasi hajasema anataka kuniacha, anataka tuoane!

55. MRS. MARAGA: (**sarcastic sneer and laughter**) Mwafrika kamili!.

56. MR. MARAGA: (**authoritative**) Mama Linda! Usisahau mimi pia ni mwanamume wa Kiafrika. Nafhamu kweli mambo yamebadilika ndiyo sababu ya kutaka Linda aendelee na masomo yake ya Uakili. Linda, Mimi na Mamako hatuna dhamira ya kukutengenisha na Chivasi. Tunachotaka ni kuona ukiwa na maisha mazuri na sio kama sisi! Na hii itawezekana tu ikiwa utasafiri kwenda Ulaya. Huko utapata elimu bora, waalimu wazuri na pia kutangamana na wanafunzi werevu zaidi...

57. LINDA: (**cuts him short**) Lakini naweza kuendelea na masomo yangu hapa nyumbani. Kwanini unipeleke nchi ya baridi Baba? Miaka mitatu bila kumuona Chivasi....Ndiyo nitarudi na shahada ya Digrii, lakini naweza pia kumkosa mpenzi wangu ambaye nimemfahamu tangu utotoni. Hiyo ni haki kweli?

58. MRS. MARAGA: (**cold and hard**) Linda, Mimi na Babako tumejaribu kadri ya uwezo wetu kuona kwamba unasafiri kwenda kusomea Ulaya. Tumetumia akiba yetu yote kugharamia elimu yako. Hivyo kulinganisha juhudi zetu na uhusiano wako wa kimapenzi na Chivasi, huko ni kututusi.

- 59. MR. MARAGA:** Mamako anasema ukweli Linda. Hapa nyumbani hakuna nafasi nyingi za kujiendeleza. Lakini ukifanya bidii katika masomo yako, mambo yatabadilika. Nafasi za ajira zitakufuata tu, tena nyingi za kipato cha juu. Na nani ajuae, labda utapata mchumba mwingine huko. Hebu fikiria kwa makini sana, kwani maisha yako yamo mikononi mwako binti yangu!.
- 60. LINDA:** Na Chivasi Je? Aliahidi kwamba ataniona pindi nitakaporudi. Sasa nitafanyaje?
- 61. MRS. MARAGA:** Mwambie utampa majibu utakaporudi. Na hii asiandike kwenye ukarasa wake wa Facebook.
- 62. MR. MARAGA:** Nini na ukarasa wa Facebook enyi watoto? Linda, wewe ni mtu mzima sasa. Hebu jaribu kufikiria kama mtu mzima!

OUTRO:

Na kwa maneno hayo ya busara kutoka kwa Bw. Maraga ndipo tunapofika mwisho wa kipindi hiki cha kwanza cha Noa Bongo jenga Maisha yako kuhusu Uhamiaji wa barani Ulaya. Je! Linda ataamua vipi kuhusu suala la uhusiano wake wa kimapenzi na Chivasi? Nini kinachomsubiri Ulaya anakokwenda kwa masomo zaidi? Pia usimsahau rafiki yetu Farahani, kutoka Afrika Kaskazini. Je! Ataamua kwamba liwe liwalo na kuhamia Ulaya? Kwa mengi zaidi ungana nasi katika kipindi cha pili kinachofuata. Pia unaweza

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”
Episode 1: “Dreams of a Sweet Tomorrow”
Author: Chrispin Mwakideu
Editors: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann
Kisuaheli: Erick Ponda

kuungana nasi kwenye mjadala wazi kupitia mtandao wetu tunapojaribu kulijadilia suala la. “Je ni kweli kwamba Vijana hawana maisha mema Barani Afrika?” Na pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa dw-world.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.